

**USEMEZANO KATIKA UMALENGA WA KISWAHILI:
MFANO WA TAARAB**

Na

Issa Yusuf Mwamzandi

**Tasnifu Inayowasilishwa Kutimiza Mahitaji ya
Shahada ya Uzamifu, Kiswahili
(Doctor of Philosophy)**

**Katika Idara ya Lugha na Isimu
Chuo Kikuu Cha Egerton, KENYA.**

EULIB



021 050

X

2002

EGERTON UNIVERSITY LIBRARY

UUNGAMAJI

Tasnifu hii ni kazi yangu mwenyewe na haijawahi kuwasilishwa kwa mahitaji ya shahada katika Chuo Kikuu chochote kile. Ni kosa kutoa nakala ya tasnifu hii bila idhini ya mwandishi na/au Chuo Kikuu cha Egerton.

Mwamzandi
ISSA YUSUF MWAMZANDI

8.10.02

TAREHE

Tasnifu hii imewasilishwa kwa minajili ya kutahiniwa kwa ridhaa yetu tulioteuliwa rasmi na Chuo Kikuu cha Egerton kama wasimamizi.

Prof. Rocha M. Chimera
for PROF. ROCHA M. CHIMERAH
CHUO KIKUU CHA EGERTON
IDARA YA LUGHA NA ISIMU
S.L.P. 536, NJORO-KENYA.

9.10.02

TAREHE

Dkt. Mwenda Ntarangwi
for DKT. MWENDA NTARANGWI
CHUO KIKUU CHA EGERTON
IDARA YA LUGHA NA ISIMU
S.L.P. 536, NJORO-KENYA.

9/10/2002

TAREHE

TABARUKU

Kwa mke wangu Mwanarusi na binti zetu N'wandinda Aisha na Tsuzi Shamsa.

SHUKRANI

Ufanisi wa tasnifu hii ni mchango wa watu wengi ambao kwa pamoja ningependa kuwashukuru. Awali, natanguliza shukrani zangu za dhati kwa wasimamizi wangu Profesa Rocha M. Chimerah na Dkt. Mwenda Ntarangwi. Kwa hakika kazi waliofanya walimu hawa haiwezi ikakadirika. Kwao nimejifunza mengi na kuusana upekuzi wangu wa mambo. Nimefaidika kwao sio kimawazo tu bali hata kwa vitabu vyao adimu ambavyo sidhani vinapatikana popote katika maktaba zetu nchini.

Pili, ningependa kuwashukuru wasimamizi wa Chuo Kikuu cha Egerton kwa kunitunukia nafasi ya kujiendeleza kimasomo. Fedha nilizopokea kutoka kwa Chuo Kikuu cha Egerton zimeniwezesha kuukamilisha utafiti wangu hasa nikiwa nyanjani huko Mombasa.

Sambamba na wakuu wa chuo napenda pia kumshukuru mkuu wa Idara ya Lugha na Isimu, Bi. Catherine Kitetu kwa kunijulia hali kila mara na kunipa moyo wa kuendelea na utafiti. Mara nyingi nilifaidika na ushauri wake kuhusiana na matatizo na mikabala ya kiutafiti. Nashukuru sana shangazi.

Walimu wenzangu wa Idara ya Lugha na Isimu, Egerton pia wanastahili pongezi. Mawazo niliyopata kwao si haba. Hawa ni mashahidi waliopata kuuona mwanzo wa utafiti huu na kuchangia kimawazo. Hulusani, ningependa kuwataja Mdkt. Karisa Beja, Aswani Buliba, Aggrey Were-Mwaro (marehemu), John Kimemia, Walimu Onyango Ogolla, Furaha Chai, E. Mohochi, Daudi Chacha, Gwachi Mayaka, Anne Juma, E. Kirigia, Rutere Mugambi, Anne Mugambi, Margaret Njeru, Nderitu Karanu na Joyce Laboso.

Nitamuenzi Profesa Kimani Njogu kwa kunipa ilhamu ya kuyazamia masemezano. Huyu ni mwalimu wangu wa kwanza kuhusu uwanja huu na vitabu alivyoniibebesha ili nimuelewe Bakhtin vilinifaa sana.

Chama cha CHAKITA-KENYA nacho nakipa kongole kwa kuandaa semina za kila mwaka. Kwa hakika semina hizi zilikuwa jukwaa langu adimu la kuwasilisha mawazo yaliyomo katika tasnifu hii. Mchango niliopata kutoka kwa washiriki ulinifaa sana.

Nikiwa Jijini Mombasa, niliwahi kupata ushauri pia kutoka kwa wakala wangu. Muadhamu Ahmad Sheikh Nabhany alinichukulia kama mtoto wake nikiwa huko Mombasa. Huyu aliniongoza kwa watu mashuhuri ambao ningeweza kuwaendea kwa lengo la kupata habari nilizolenga kukusanya. Ahmad Nasir Juma Bhalo naye alinifaa kwa kunieleza mengi kuhusu tarehe ya ushairi wa Kiswahili na wakoloni wa Jiji la Mombasa. Kache Gungu wa *Bhalo and Party*, alinipa habari muhimu kuhusu tamasha za kikundi chao. Vilevile, wenye duka la *Mbwana Radio Service* walithibitisha ukarimu wao kwa wageni kwa kuviweka vitabu vyao wazi ili nijionee mwenyewe wapi ningenda kujionea tamasha za taarab. Tamasha nyingi za taarab nilizohudhuria zilifanikishwa na wenye duka hili. Abduli na Hassan nao nawashukuru kwa kunipenyeza kwenye “vichochoro” vyao vya Mji wa Kale, Mombasa.

Vilevile, napenda niwashukuru wazazi wangu kwa kunilea na kunielimisha. Kwenu nina fahari kubwa na sidhani hilo ni jambo la mjadala. Nawaombea jicho la hasidi lisiwaone!

Kakangu Mohamed na dada zangu Riziki, Sherry na Gago nao wanastahili pongezi kwa mchango wao. Daima nitaukumbuka usaidizi wenu mlipokuwa nyumbani kwangu hapa Njoro. Dada Zuhura anastahili pongezi za kipekee kwa kunisaidia katika kunakili mamia ya nyimbo za taarab. Kwa uvumilifu na satuwa uliifanya kazi hiyo kana kwamba ni yako.

Mwisho ni kwa mke wangu Mwanarusi ambaye uvumilivu na ushauri wake ulinifaa sana. Kwa hakika umekuwa mtu wa kutegemeeka na wa kuniliwaza kila nilipojikuta kwenye hali za uvunjifu. Nakushukuru pia kwa kuwaangalia mabinti zetu wakati wa pata shika zangu.

Kwenu N'wandinda na Tsuzi, msikate tamaa katika rehema za Mungu, daima atawaongoza na atawabariki.

UFAFANUZI WA ISTILAHU

Katika utafiti huu, nimetumia istilahi zifuatazo kwa maana maalum kama nilivyopendekeza hapa chini.

Usemezano:

Kimsingi, istilahi hii inahusu maingiliano kati ya watu wawili. Ingawa hivyo masemezano yanayosisitizwa katika kazi hii si lazima yawe ya ana kwa ana. Badala yake, yatarejelea hali ya kuwepo kwa usemi ambao unajibu usemi wa awali, huku ukitarajia jawabu kutoka kwa usemi utakaofuata. Hali hizi mbili za kujibu na kutarajia majibu za usemi wowote zinaweza kudhihirika katika usemi mmoja. Usemezano wa tasnifu unahusu mijadala kuhusu semi hizo ambazo zimeibuka kutoka miktadha mbalimbali ya kijamii, na vilevile, ya kiitikadi. Hatimaye, usemezano unaendeleza sifa kuwa maana na mawasiliano huenda sambamba na tajriba za msemaji, hivi kwamba hatuwezi kuwa na aina moja ya maana au mawasiliano. Semi za watu tofauti kama vile washairi, waimbaji, hadhira, na hata miktadha inamotendewa taarab imebainika kama usemi mmoja unaodhihirisha tofauti za kusemezano.

Uzungumzi Nafsi:

Katika utafiti huu, istilahi hii imerejelea matini ambazo kuna sauti moja tu inayotokana na harakati za kugandamizwa kwa sauti nyingine zinazopigania kusikika. Kwa kutumia mifano kemkem ya taarab, tasnifu hii imepinga rai kuwa ushairi wa Waswahili ni uzungumzi nafsi na badala yake kupendekeza kuwa ni masemezano ya watu wa aila mbalimbali katika jamii.

Utendaji:

Utendaji unahusu maswala ya uzalishaji na uwasilishaji wa kazi inayotendwa kwenye jukwaa kwa kuishirikisha hadhira. Katika utafiti huu, nimejishughulisha na taarab ambayo hutendwa mbele ya hadhira. Nimeuangalia utendaji kama usemi ulioundwa kimjadala. Nimedhihirisha kuwa utendaji unaweza ukawa usemi kutokana na aina kadhaa za maana na mawasiliano zinazoweza kujitokeza kwa upande wa hadhira na washiriki wengine wa taarab.

Heteroglosia

Nimeitumia dhana hii kurejelea semi zilizochotwa kutoka maeneo tofauti tofauti ya kijamii, kiitikadi na hata kiisimu. Katika tasnifu, heteroglosia inajikita kuchunguza semi au 'lugha' zisizokuwa za kishairi ambazo huingizwa kisitiari katika nyimbo za taarab. Kwa mfano, imebainishwa katika tasnifu jinsi nyimbo za taarab zinavyoingiza semi au 'lugha' zinazofungamanishwa na kazi za kijamii kama vile udaktari, udereva, au sajili za barua, mazungumzo ya simu, na hata matumizi ya tanzu za fasihi simulizi kama vile, vitendawili na misemo. Uamilifu wa semi hizo katika kufanikisha usemezano na mawasiliano ya kisitiari ndilo jambo kuu lililoendelezwa na dhana hii ya heteroglosia.

Shani:

Nimeitumia dhana ya shani kwa azma ya kurejelea jumla ya mambo ambayo yanakiuka miiko, mbeko na ufasaha wa mazungumzo ya Waswahili. Nimeitumia dhana hii kurejelea miktadha maalum ya taarab ambayo inaruhusu kuvunjwa kwa miiko na mbeko hizo. Wakati huo, maisha katika taarab hudhihirika yakiwa 'kinyume mbele.' Ingawa hivyo, kuvunjwa kwa miiko hiyo huwa na lengo fulani, hasa katika kuyasarifu upya

maisha katika jamii. Kwa mfano, imebainishwa na tasnifu kuwa taarab hutoa wasaa wa kutendwa kwa shani na, hivyo basi, kutoa fursa ya kupingwa kwa itikadi kuu za kijamii.

Miktadha ya Kijamii na Kiitikadi:

Dhana hizi mbili zimetumiwa kuakisi kwamba masemezano hayatokani na ombwe tupu. Badala yake, dhana hizi zinaashiria kuwepo kwa nguvu mbalimbali za kijamii ambazo zinaipatia taarab kipaza sauti cha kuzijadili nguvu hizo inapotendwa. Kama aina ya usemi, taarab inajikita katika miktadha mahsusi ya kijamii na inazungumzia maswala ya kisiasa, kiuchumi, kiutamaduni na hata kiitikadi. Tasnifu imefungamanisha semi za taarab na watu wanaotoka katika ngazi mbalimbali za jamii. Wasemaji hao wameleta athari zao za kijamii na kiitikadi ambazo zinaelekea kukinzana na wakati mwingine zikiwa na mwelekeo sawa.

MUHTASARI WA TASNIFU

Tasnifu hii imechunguza kipengele cha usemezano kama mkakati wa mawasiliano katika umalenga wa Waswahili. Kwa kutumia taarab kama kielelezo nimefafanua na kuonyesha jinsi masemezano hayo yanavyosukwa na kuwa msingi wa mawasiliano miongoni mwa washiriki wa sanaa hii. Waasisi wa nadharia ya usemezano, hasa Bakhtin na wenzake, wamependekeza kwamba usemezano ni sifa inayojidhihirisha tu katika riwaya na kwamba haijitokezi katika utanzu wa ushairi. Kinyume na maoni hayo, tasnifu hii imeonyesha, kwa mifano kemkem, kwamba dhana ya usemezano imesakini katika ushairi pia. Kwa hivyo, ushairi wa Kiswahili wapaswa kutazamwa kama utanzu ulio na jadi pevu na uwezo wa kujadili mada yoyote ile bila udhia wowote unaotokana na kuzingatiwa kwa arudhi.

Katika sura ya kwanza dhana ya usemezano imechunguzwa kwa kuangazia mchango wa waasisi wa nadharia ya usemezano hasa ule wa muasisi mkuu Bakhtin na wenzake, wakiwemo Lodge (1990) na Dentith (1995). Hususani, ugiligili unaofungamana na usemezano umebainishwa. Kama walivyotahadharisha waasisi wa usemezano, dhana hii ina hatari ya kutoa picha ya watu wawili wanaojibizana ana kwa ana. Hii ni aina moja ya usemezano inayokubalika lakini sio aina ya kipekee. Kwa kutoa mfano wa ushairi wa Kiswahili, nimefafanua jinsi dhana hii inavyoweza kupanuliwa na kushirikisha semi zinazoibuka kama maoni badalia ya hali mbalimbali za kiuchumi, kisiasa, kijamii, kiutamaduni na hata kiitikadi. Aidha msingi wa usemezano katika jadi ya umalenga wa Waswahili umewekwa hasa tunapozingatia kwamba ushairi ndiyo njia kongwe zaidi ya mawasiliano miongoni mwa wanajamii hawa. Ari ya kuuchunguza ushairi wa Kiswahili kwa ujumla inatokana na ukweli kwamba kimsingi, taarab ni ushairi.

Sura ya pili inachanganua dhana na umbo la usemezano na mawasiliano katika taarab. Ili kulifikia lengo hilo, nimeigawanya sura hii katika sehemu mbili kuu zinazoathiriana na kujengana. Sehemu ya kwanza imezamia semi au mchango wa washiriki wakuu wa taarab katika kuyasana masemezano na mawasiliano. Mwelekeo wa tasnifu ni kwamba kila mshiriki ni msemaji anayejaribu kutoa maana kwa wimbo wa taarab hivi kwamba 'maana kadhaa' zinazozuka zimechunguzwa. Nayo sehemu ya pili imezingatia aina na ruwaza mahsusi za usemezano zinazojitokeza katika nyimbo za taarab. Sehemu hizi mbili zinaeleza kwa urefu uchanganu uliopo katika usemezano na mawasiliano ya sanaa hii.

Sura ya tatu imechunguza kipengele cha utendaji kwa kuzingatia nyimbo mbalimbali zinazowiana na miktadha ya kimatumizi ili kudhihirisha tofauti za usemezano na mawasiliano yanayoibuka. Ni rai ya tasnifu kuwa miktadha ya kimatumizi ya taarab, ikiwemo arusi, mikutano ya kisiasa, harambee na kuwakaribisha wageni, ina nafasi maalum ya kusana aina maalum za usemezano. Hususani, nyimbo zenye fungamano la moja kwa moja na miktadha hii ya kimatumizi zimechanganuliwa kwa lengo la kuona jinsi masemezano yanavyofana au pia kutingwa. Masemezano adimu yanayogusia vyama vya kisiasa nchini Kenya, jinsia, na hata matumizi ya taarab kama kivutio cha hadhira katika harambee yamechunguzwa.

Sura ya nne imewasilishwa kwa kuzingatia kwamba miktadha ya kimatumizi haitoshi kueleza kwa kina baadhi ya nyimbo za taarab ambazo aghalabu hutumia miktadha mipana zaidi. Nyimbo za shani huwa zinalenga miktadha ya kuwazika na kufikirika ambayo huenda ikazifanya nyimbo hizo zisieleweke iwapo zitafungamanishwa na miktadha ya kimatumizi. Kama kipengele cha kiusemezano, shani katika taarab yasaikia kuweka hadharani mambo ambayo yangezusha shauku na fedheha katika muktadha wa kawaida. Kwa mfano, ni kupitia

kipengele cha shani ambapo wanajamii wanapata fursa ya kuwasaili watawala bila kikomo huku waajiriwa wakipinga waziwazi dhuluma wanazofanyiwa na waajiri. Katika sura hii, maswala yanayobainisha maisha yakiwa 'kinyume mbele' yamepewa ufafanuzi.

Sura ya tano imechunguza matumizi ya heteroglosia kama kipengele cha usemezano. Kwa muhtasari, sura hii imezamia umbuji wa nyimbo za taarab hasa katika kutumia heteroglosia iliyochumwa kutoka maeneo mbalimbali ya kijamii. Aghalabu, heteroglosia hiyo imebainika kama sitiari zinazotumiwa kimakusudi na washiriki wa taarab na ni msingi muhimu wa kukweza masemezano na mawasiliano yaliyomo katika nyimbo.

Mwisho, sura ya sita imetoa matamko mahsusi kuhusu ruwaza mbalimbali za masemezano na mawasiliano yanayojitokeza katika taarab. Muhtasari unaofafanua dhana ya usemezano katika taarab umetolewa huku tasnifu ikichukua msimamo mahsusi kuhusu usemezano wa Waswahili. Marekebisho na mapendekezo ya hapa na pale kuhusu usemezano wa taarab yametolewa. Hatimaye, mapendekezo kuhusu maeneo mengine ambayo yanahitaji kutafitiwa yametolewa.